



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 12 Mei, 2022

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

157. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, ni wajasiriamali wangapi na watu wenye mahitaji maalum walionufaika na kuweza kujitegemea kufikia hatua ya kutengeneza ajira mpya kwa wengine.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

78. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa katika Ripoti ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka wa fedha 2015/2016 imemripoti mwekezaji wa Kiwanda cha Sukari Mahonda kuwa anadaiwa kodi ya ardhi yenye thamani ya Dola za Kimarekani 2,629,998 kwa maeneo mbali mbali aliyokodi. Na kwa kuwa Kamati ya

PAC ya Baraza la Wawakilishi kwenye Ripoti yake ya mwezi wa Februari, 2019 iliitaka Kamisheni ya Ardhi kwa kushirikiana na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kufuatilia malipo ya kodi hiyo.

- (a) Je, hadi hivi sasa Kiwanda cha Sukari Mahonda kimekamilisha deni lake hilo.
- (b) Kama deni bado lipo, Serikali ina mpango gani juu ya Mwekezaji huyo kulipa kodi hilo.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

117. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali inastahili pongezi kwa kutambua uwepo wa vijiji vya Jitenge na Tundaua ndani ya jimbo la Pandani na kuvipelekea baadhi ya huduma za kibinaadamu. Hata hivyo, kwa siku za karibuni, vijiji vya Jitenge na Tundaua vimesahauliwa sana na kukosa huduma muhimu za kimaendeleo zikiwemo huduma za barabara.

- (a) Je, ni barabara zipi rasmi zinazotambulika na Serikali za kuingilia vijiji vya Jitenge na Tundaua ndani ya jimbo la Pandani.
- (b) Je, ni lini Serikali itazitengeneza barabara zinazoingia Jitenge na Tundaua kutoka barabara kuu ili ziweze angalau kusafirisha wajawazito ambao mara nyingi hujifungulia njiani.
- (c) Je, ni lini katika historia ya Zanzibar, Serikali iliwahi kutengeneza barabara za kuingilia vijiji vya Jitenge na Tundaua ndani ya jimbo la Pandani.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

106. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa skuli ya Ali Khamis Camp iliyopo Vitongoji zaidi ya asilimia 80 ya wanafunzi wake ni watoto wa raia wa nchi hii yaani wakwenzi na wakulima, na kwa kuwa jeshi la wananchi kwa kadri ya uwezo wao linajitahidi kujenga madarasa pamoja na mabweni ya kulaliya wanafunzi, ingawa si kwa kiwango cha kutosheleza pamoja na kiwango kinachohitajika kwa maisha ya kileo.

Je, kuna siku Serikali yetu itaonyesha jicho la huruma angalau kuwasaidia ujenzi wa madarasa katika skuli hii ya wapiganaji wetu.

118. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali inastahili pongezi kwa kutambua uwepo wa vijiji vya Jitenge na Tundaua ndani ya jimbo la Pandani na kuvipelekea baadhi ya huduma za kibinaadamu. Hata hivyo, kwa siku za karibuni, vijiji vya Jitenge na Tundaua vimesahauliwa sana na kukosa huduma muhimu za kimaendeleo zikiwemo huduma za skuli.

- (a) Je, ni skuli zipi rasmi za maandalizi na msingi zinazotambulika na Serikali zimekusudiwa kutoa huduma kwa watoto wadogo wa vijiji vya Jitenge na Tundaua ndani ya Jimbo la Pandani.
- (b) Je, ni lini Serikali itawapatia watoto wa Jitenge na Tundaua skuli za maandalizi na msingi ili watoto hao waweze kupata elimu bila ya kuhatarisha maisha yao.
- (c) Je, ni lini katika historia ya Zanzibar, Serikali iliwahi kuwa na mpango wa kuwajengea skuli za maandalizi na msingi watoto wadogo wa vijiji vya Jitenge na Tundaua ndani ya jimbo la Pandani.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
12 Mei, 2022.


(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA